
WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

# JARIDA LA UTABIRI WA HALI YA MAJI MTO RUVU







Imeandaliwa na;

**Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu**


P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania

Phone: 0800114031 / 0800114032

E-mail: barua@wrbwb.go.tz

Website: www.wrbwb.go.tz


Januari 2026


# 1. UTANGULIZI

**Yaliyomo**


1. UTANGULIZI
2. UTABIRI WA HALI YA MAJI
3. HITIMISHO


Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kuzingatia vituo vilivopo katika Catchment (**Kielelezo Na.1**) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 26 Januari, 2026 hadi 05 Februari 2026. Utabiri huu unalenga kuwezesha wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kufahamu mwenendo wa wingi wa maji katika mto huo.

waweze kujua hali ya mwenendo wa wingi wa maji. Aidha, utabiri huu umezingatia utabiri wa hali ya mvua na Joto zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).





Kielelezo Na.1: Vituo vilivyotumika kufanya utabiri wa wingi wa Maji katika *Catchment* ya Mto Ruvu

## 2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu umefanyika kwa siku kumi zijazo kuanzia tarehe 26 Januari, 2026 hadi 26 Februari, 2026 kama inavyoonekana katika Jendwali Na. 1; -

**Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu katika kituo cha *Ruvu river at* Morogoro road bridge (1H8A).**

| Jina la Mto | Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji | Kielelezo |
|---|---|---|
| *Ruvu river at Morogoro road bridge (1H8A)* | Utabiri unaonyesha wingi wa maji kwa sasa uko chini ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009-2024). Aidha, kiwango cha maji kinaendelea kupungua kutokana na upungufu wa mvua katika safu ya Milima ya Uluguru hatahivyo, kiasi kilichopo kwa sasa na siku kumi zijazo ni himilivu na kinatosheleza mahitaji ya sekta mbalimbali ikiwemo mahitaji ya maji majumbani katika Mitambo ya DAWASA ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Mahitaji uwandani ni mita za ujazo sita (6) kwa sekunde (**jendwali Na.1**). |  |

## 3. HITIMISHO

Bodi inapenda kuwashauri watumiaji wa Maji katika sekta ya Kilimo, Mifugo, Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kutumia maji yalipo kwa ufanisi na kuthibiti upotevu wa maji. Aidha Bodi inazishauri sekta hizi kuwa na njia mbadala ya upatikanaji wa maji ikiwemo visima virefu endapo kutatokea upungufu wa maji katika Mto Ruvu.

Bodi itaendelea kutoa taarifa ya mwenendo wa wingi wa maji kila baada ya siku kumi na kuwahabarisha wanufaika na Mto Ruvu ili waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa siku zijazo.